

# Tupigane dhidi ya mbu

Mwongozo wa mwelekezi
**SC Johnson Guardian™**

# Sehemu Za Huu Mwongozo


| | |
|---|---|
| **Maagizo** | **3** |
| **Maelezo ya Malaria** | **6** |
| **Maelezo kuhusu SC Johnson Guardian™** | **20** |
| **Hatua zinazofuata** | **33** |

# Maagizo ya Mwongozo wa mwelekezi



**Hiki kitabu ni mwelekezo kwa wafanyikazi wa afya ya umma na waelekezi wengine kutumia kwa kutoa elimu na katika usambazaji wa Guardian™.**

Tumia mwongozo huu kuelekeza majadiliano kuhusu njia za kuzuia na kupunguza malaria, kwa makundi madogo madogo na pia manyumbani. Kupitia majadiliano haya, lenga kubadilisha tabia, na kujulisha jamii kuhusu mbinu za kumaliza malaria.

## Vitu ambavyo utahitaji



Huu mwongozo



Karatasi zenye ujumbe kuhusu Guardian™




Karatasi ya kupiga hesabu za usambazaji




Bidhaa za kutosha nambari ya watu unaotembelea




Kipimo cha mkanda na kamba ya urefu wa mita moja (ikiwa inapatikana)



Kalamu

## Utatumia vipi huu mwongozo



Kufanya mazungumzo na makundi madogo



Kufanya mazungumzo na watu kwa nyumba zao

# Makundi madogo: Mwongozo wa mazungumzo


MWELEKEZI

**Lengo**
Kuwasilisha mafunzo ya jumla kuhusu malaria, bidhaa ya Guardian™, na mpangilio wa kupeana bidhaa.

Pitia maelezo kuhusu usalama

## Kabla ya mazungumzo

1. **Kufanya mazungumzo na watu kwa nyumba zao**
2. **Kusanya vifaa vyote vinavyohitajika mapema**





Ukubwa wa kikundi unaeza kua tofauti kulingana na jamii

## Unapoongoza mazungumzo

- Hakikisha watu wanaonekana ili kupeana nafasi ya mawasiliano kwa uwazi kwa kupanga watu wakae kwa mviringo.
- Anza mazungumzo kwa kuwaamkua washiriki, kuwashukuru kwa uwepo wao, na kupeana nafasi ya kujuliana hali.
- Tangulisha mada ya majadiliano na ukaribishe washiriki kuchangia changamoto ambazo wamepitia kujichunga pamoja na familia zao kutokana na malaria.
- Chochea ushirikiano kwa kuwapa washiriki motisha ya kuchangia maoni, maswali na fikira zao.
- Tilia maanani maswali ya washiriki, ukihakikisha maswali yote yanajibiwa kabla umalizie mazungumzo.
- Tumia lugha inayoeleweka ili kuhakikisha kila mhuduriaji anaelewa.
- Peana muda wa kutosha kwa maoni na maswali ya washiriki. Ama, fanya maonyesho ndani ya nyumba ili kuonyesha njia tofauti za kupima, tumia ile karatasi ya kupiga hesabu, na uonyeshe wapi na jinsi ya kutundika GuardianTM.
- Malizia mazungumzo kwa kufupisha pointi kuu, ukipeana shukrani kwa washiriki wote, na kupanga tarehe za kupeana bidhaa kwa maboma.
- **Hiari:** fanya maonyesho kwa boma ya njia tofauti za kupima, tumia karatasi za kufanya hesabu, na aje/wapi wanafaa kutundika Guardian™.
- Malizia kwa:
    - Fupisha mazungumzo na jumbe kuu
    - Kushukuru kila mtu
    - Kukubaliana tarehe za kupeana bidhaa kwa maboma

# Kutembelea manyumba

MWELEKEZI


## Kusudi


Kupeana mafundisho jumla kuhusu malaria, bidhaa ya Guardian™, na maagizo matumizi/kupeana.

Pitia habari za usalama na ujibu maswali yoyote.

## Kabla ya kila ziara

1. **Hakikisha na wenye boma mapema**
2. **Tayarisha vifaa vyote unavyohitaji:**



## Peana bidhaa

- Kama kawaida kwa utamaduni wetu, bisha, amkua, na uulize uliowatembelea wakukaribishe.
- Washukuru kwa wakati wao, waambie sababu ya ziara yako na mada ambayo unazungumzia.
- Tumia kurasa za huu mwelekezo kupitia malaria, jinsi inavyoenea, na jinsi ya kujibu dalili.
- Pitia habari kuhusu bidhaa na upeane bidhaa.
- Malizia mazungumzo kwa kuwashukuru kwa kuchukua muda wao kuongea na wewe, waahidi kua unapatikana ikiwa kuna maswali au wasiwasi kuhusu Guardian™ au jinsi ya kuitumia.

## Distribute product

- Jaza karatasi ya bidhaa pamoja na mkuu wa kaya.
- Kisha, peana idadi sahihi ya bidhaa baada ya maswali yote kujibiwa.

# Malaria ni ugonjwa wa aina gani?






# Malaria ni ugonjwa wa aina gani?



Karatasi ya kuonyesha mteja



Ni nini mnaeza zungumzia

**Malaria ni nini?**

- Malaria ni ugonjwa unaosababishwa na kimelea kinachoitwa *Plasmodium*.
- Malaria inaenezwa na kuumwa na kuumwa na aina ya mbu inayoitwa *Anopheles*.

**Watu ambao wako na hatari kubwa ya malaria**

- Japo kila mtu anaweza pata malaria, watu ambao wako kwa hatari kubwa ya malaria ni kama: kina mama wajawazito na watoto chini ya miaka tano, ambao haswa wako kwa hatari kwa kesi kali za huu ugonjwa. Hata maambukizi kidogo tu kwa watoto inaeza fikia kua hali mbaya, ambayo inaweza sababisha vifo.

# Mbu wa kueneza malaria



# Malaria ni ugonjwa wa aina gani?

MWELEKEZI

Karatasi ya kuonyesha mteja




Ni nini mnaeza zungumzia

**Ni aina gani ya mbu hueneza malaria?**

- Kuna aina mingi tofauti za mbu.
- Mbu za *Anopheles* ndio pekee zinaeza eneza malaria.
- *Anopheles* ni tofauti kutoka kwa mbu wengine kwa sababu ya bawa zao za rangi nyeupe na nyeusi.
- Mbu wa kusababisha malaria sanasana huuma katikati ya jioni na asubuhi.
- Kuhepa kuumwa na mbu wakati huu ni muhimu sana kwa kuzuia malaria.


# Uenezaji wa malaria



# Malaria ni ugonjwa wa aina gani?

MWELEKEZI

Karatasi ya kuonyesha mteja




Ni nini mnaeza zungumzia

**Unajua jinsi malaria inaenezwa?**

- Malaria inaenezwa kwa kuumwa na mbu.
- Mbu anapouma mtu aliye na malaria anachukua damu yake pamoja na vimelea vya malaria (*Plasmodium*).
- Vimelea vya malaria hukua na kuzaana ndani ya mbu.
- Kisha, mbu aliyeambukizwa anapouma mtu mwingine, inaweza pitisha hivyo vimelea kwa huyo mtu.
- Mbu mmoja aliyeambukizwa anaweza peana malaria kwa watu wengi.


# Uzazi wa mbu wa kueneza malaria



# Malaria ni ugonjwa wa aina gani?



Karatasi ya kuonyesha mteja



Ni nini mnaeza zungumzia

**Unajua jinsi mbu wanaosababisha malaria huzaana?**

- Mbu wa kusababisha malaria huzaana kwa njia ifuatayo
- Mbu wanahitaji maji yaliyotuama kutaga mayai yao.
- Mbu wazima wa kike hutaga mayai yao kwa maji ya bwawa yaliyotuama, maji yaliyotekwa kwa mitungi wazi, ama kwa maji yanayosonga pole pole sana.
- Baada ya kadri ya siku mbili tatu, mayai huangua, na kutoa mbu wadogo.
- Hao mbu wapya wanabaki kwa maji kula.
- Kwa siku chache, mbu hukua zaidi kabla waweze kuruka na kutawanyika."

# Dalili za malaria


Joto jingi


Kutetemeka


Kuumwa na kichwa


Uchovu


Kujihisi kutapika


Uchungu

# Je, malaria ni ugonjwa wa aina gani?



Karatasi ya kuonyesha mteja




*Wakati mtu hajiskii vizuri na ana joto jingi, chanzo chake hua sio dhahiri, kwani magonjwa mengi huonyesha joto jingi kama dalili yao ya kwanza.*

## Ni nini mnaeza zungumzia

**Dalili za malaria**

- Joto jingi na baridi: unahisi joto jingi ikiambatana na baridi na kutetemeka.
- Kuumwa na kichwa sana: unaumwa na kichwa kwa uchungu sana.
- Kuchoka sana: kuhisi uchovu sana unapoamka, licha ya kua na usingizi mrefu.
- Kuumwa na mwili na uchungu: unaumwa na mwili mzima, sazingine na uchungu mwingi mgongoni.
- Kujihisi kutapika na kutapika: unajihisi kutapika na unatapika pia.
- **Mtu akiwa mgonjwa na ana joto jingi, inaweza kua ngumu kujua sababu, magonjwa mengi huonyesha joto jingi kama dalili ya kwanza**

## Uliza maswali kuhusu dalili za malaria

- Unajua dalili zozote za malaria?
- Unajua dalili za malaria ni zipi?
- Wewe ama mtu yeyote kwa familia yako mmeugua malaria?
- Uliona dalili gani ulipokua na malaria?
- Dalili za malaria zinaweza tofautiana kutoka kwa mtu mmoja hadi mwingine?
- Unafaa upimwe punde tu unapohisi dalili tofauti?
- Ukipatikana na malaria, unafaa ukubali matibabu?


# Dalili za malaria kali



Kukosa hamu ya chakula



Kupoteza fahamu



Matamshi kutokana na joto jingi



Ukosefu wa damu

# Dalili za malaria kali

MWELEKEZI

Karatasi ya kuonyesha mteja





Ni nini mnaeza zungumzia

**Dalili za malaria kali**

- **Joto jingi:** Joto inayozidi nyuzi joto 39
- **Kubadili tabia:** Kubadilisha tabia kutokana na joto jingi, kama vile kuchanganyikiwa, ugumu wa kulala, kushindwa kutambua vitu, kushindwa kukaa bila kusaidiwa, kushindwa kuongea, na kukosa kutambua familia.
- **Kutapika mfulilizo:** Kuendelea kutapika na kushindwa kumeza dawa
- **Kukosa hamu ya kukula na kunywa:** Kukosa kula au kunywa
- **Ukosefu wa damu:** Upungufu mkubwa kwa mishipa ya damu
- **Kukojoa kusio kawaida:** Mkojo kidogo sana au hakuna kabisa, saa zingine mkojo wenye rangi nyeusi
- **Upungufu wa maji mwilini:** Mwonekano wa kunyauka na macho yasiyo na nguvu kutokana na ukosefu wa maji mwilini.
- **Kuendesha sana:** Kuendesha bila kuacha
- **Kutokwa damu kusio kwa kawaida:** Kutoka damu kwenye pua, fizi, au sehemu zingine za mwili.

# Hua unafanya nini ukiwa na dalili za malaria





# Hua unafanya nini ukiwa na dalili za malaria

MWELEKEZI

Karatasi ya kuonyesha mteja




Ni nini mnaeza zungumzia

**Ikiwa wewe au familia yako mna dalili za malaria**


- **Tafuta huduma ya afya ya dharura:** Tembelea hospitali iliyo karibu au mhudumu wa afya wa kijiji upimwe na, kama inahitajika, anza matibabu moja kwa moja.
- **Epuka kuchelewa:** Matibabu ya haraka ni muhimu. Kuchelewa kutibiwa inaweza sababisha dalili mbaya zaidi na inaweza hatarisha maisha.
- **Anza matibabu mara moja:** Ukipatikana na malaria, anza kumeza dawa ulizopewa bila kuchelewa.
- **Unafanya nini ukigundua dalili za malaria**
- **Pimwa malaria:** Familia yako imewahi pimwa malaria? Ukigundua dalili, ni muhimu upimwe mara moja.

Uliza maswali kuhusu cha kufanya unapoona dalili za malaria.

- Ni nini wewe au familia yako mnaweza fanya mkianza kugundua dalili za malaria?
- Ummewahi pimwa malaria?

# SC Johnson Guardian™






Tumia ndani ya boma yako kujikinga wewe na familia yako

Inalinda kwa hadi mwaka mmoja

**1** mwaka

Karatasi ya kuonyesha mteja




Muhimu


Unaweza peana karatasi ya maelezo kuhusu Guardian™ sasa na uambie washiriki kua wataipokea wakati wa kutembelewa nyumbani

## Habari muhimu ya kushiriki

**Kuhusu Guardian™**

- Guardian ni chombo kipya kilichotengenezwa kulinda familia yako kutokana na mbu ndani ya boma yako
- Hii spatial repellent hufanya kwa kuitundika kwa nyumba yako.
- Haihitaji kuchoma, kueka kwa stima, au kutumia betri.
- Inakulinda wewe na familia yako kwa muda wa hadi mwaka mmoja.
- Hii bidhaa haina harufu; kiungo hai kinachofukuza mbu hakionekani kwa binadamu.
- Bado kuna wezekano utaona mbu, lakini tunakuhakikishia, hii bidhaa ni maarufu kwa kuwazuia kukuuma.

# SC Johnson Mosquito Guardian™ : Habari muhimu ya kujua



Endelea kutumia neti



Weka mbali na watoto




Shika wa kando pekee



Nawa mikono na maji na sabuni baada ya kuzishika



Weka mbali na jua na mvua



Usioshe Guardian™

### Karatasi ya kuonyesha mteja






## Habari muhimu ya kushiriki

**Muhimu!**


- Bidhaa imekubalika kutumiwa kwa boma zote, pamoja na zile zina watoto, watoto wachanga, na wanawake wajawazito.
- Endelea kutumia neti kila usiku kwa ulinzi zaidi.
- Weka mbali na watoto. Hakikisha Guardian inatundikwa salama mbali na mahali watoto wadogo wanaeza fika, maana kueka chini inaweza ruhusu watoto waitoe, na hivyo kupunguza utendakazi wake.
- Shika pembeni pekee
- Nawa mikono na maji na sabuni baada ya kuzishika
- Weka mbali na miale ya jua na mvua. Kuonekana kwa jua na mvua itafupisha muda wa maisha ya bidhaa, kisha kupunguza utendakazi wake uwe chini ya mwaka mmoja.
- Usioshe bidhaa. Tofauti na neti, Guardian haifai kuoshwa, hata ikiwa chafu . Kuosha kutatoa kile kiungo kilicho hai, na kuikosesha umaarufu na pia inaweza umiza mazingira.

# Bainisha Guardian™ ngapi za kutumia









| Upana(m) \ Urefu(m) | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 | 8 | 9 | 10 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | 2 | 2 | 2 | 2 | 2 |
| 2 | 1 | 1 | 2 | 2 | 2 | 2 | 2 | 2 | 2 | 2 |
| 3 | 1 | 2 | 2 | 2 | 2 | 2 | 2 | 2 | 4 | 4 |
| 4 | 1 | 2 | 2 | 2 | 2 | 2 | 4 | 4 | 4 | 4 |
| 5 | 1 | 2 | 2 | 2 | 4 | 4 | 4 | 4 | 4 | 6 |





| Kipenyo(m) | |
|---|---|
| 2 | 1 |
| 3 | 2 |
| 4 | 2 |
| 5 | 2 |
| 6 | 4 |

## Karatasi ya kuonyesha mteja




| Upana(m) \ Urefu(m) | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 | 8 | 9 | 10 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | 2 | 2 | 2 | 2 | 2 |
| 2 | 1 | 1 | 2 | 2 | 2 | 2 | 2 | 2 | 2 | 2 |
| 3 | 1 | 2 | 2 | 2 | 2 | 2 | 2 | 2 | 4 | 4 |
| 4 | 1 | 2 | 2 | 2 | 2 | 2 | 4 | 4 | 4 | 4 |
| 5 | 1 | 2 | 2 | 2 | 4 | 4 | 4 | 4 | 4 | 6 |




| Kipenyo(m) | |
|---|---|
| 2 | 1 |
| 3 | 2 |
| 4 | 2 |
| 5 | 2 |
| 6 | 4 |

## Kumbuka

Unaweza peana karatasi ya kupiga hesabu wakati huu au uambie washiriki watajaza karatasi ya hesabu pamoja wakati wa kutembelewa nyumbani.

## Maswali ya kuzungumzia

- Unajua jinsi unaweza pima nafasi yako kwa hii bidhaa?
- Utatumia bidhaa hizi ngapi?

## Habari muhimu ya kushiriki

- Idadi ya bidhaa unazohitaji inaamuliwa na nambari ya vyumba na ukubwa wa vyumba ulivyo navyo.
- Tumia karatasi tuliyokupatia kuhesabu idadi ya biodhaa inazohitaji.
- Unaweza bainisha ukubwa wa vyumba vyako aitha kwa kutumia kipimo cha mkanda (au kamba yenye urefu wa mita moja) ama kutembea kando ya chumba (hatua kubwa ni kadhri ya mita moja)
- Ikiwa huezi fikia nafasi ya hio nyumba wakati huu, unaeza kadiria ukubwa wa chuma kwa kuifananisha na chumba ulichopima kwa kuchukua hatua.
- Baada ya kuamua ukubwa wa nyumba vyako, utapokea idadi ya bidhaa inayofaa kutumika.
- Kila chumba kinahitaji kupimwa tofauti na kuandikwa kwenye karatasi. Chumba kinatengenezwa kila mara nyumba inapogawanywa kwa nafasi tofauti - iwapo kwa ukuta au pazia/nguo. Haijalishi ikiwa kitu kinachogawa hakifiki juu ya paa/dari. Kila chumba kitahitaji idadi inayofaa ya Guardian™.

# Mahali pa kutundika Guardian™ kwa kila chumba



# Mahali pa kutundika Guardian™ kwa kila chumba

MWELEKEZI


Karatasi ya kuonyesha mteja




Habari muhimu ya kushiriki

- Guardian™ inahitaji kuekwa kwa kila chumba. Chumba kinatengenezwa kila mara nyumba inapogawanywa kwa nafasi tofauti - iwapo kwa ukuta au pazia/nguo. Haijalishi ikiwa kitu kinachogawa hakifiki juu ya paa/dari. Kila chumba kitahitaji idadi inayofaa ya Guardian™.
- Weka Guardian™ kwa usawa kwenye chumba. Ukiacha nafasi kando kando ya bidhaa.
- Usitundike bidhaa kwenye milango na madirisha. Kuweka bidhaa kwa milango na madirisha inaweza fanya kiungo hai kiende nje badala ya kulinda nyumba. Pia inaweza sababisha upepo ufanye bidhaa ianguke chini na isikue na utendakazi.
- Usitundike ama kuweka chochote mbele ya bidhaa - ikiwa nguo, picha, samani, etc. Guardian™ inahitaji kua wazi kwa nyumba ili kiungo hai kisambae kote nyumbani. Kutundika au kueka chochote mbele ya bidhaa inaweza isababisha isikue na utendakazi kwa kuzuia kuumwa na mbu.
- Bidhaa zinafaa zitundikwe kule watoto hawaezi fikia.

# Njia za kutundika Guardian™






# Njia za kutundika Guardian™



Karatasi ya kuonyesha mteja



## Habari muhimu ya kushiriki

- Unaweza kutundika Guardian™kwa urahisi kutumia bidhaa za kila siku za nyumbani
- Tumia chochote kinachopatikana kutundika Guardian™kutoka kwenye ukuta au paa, kama vile misumari, nyengo, mkanda, au kamba.
- Tafuta shimo zilizo upande wa juu wa bidhaa ya Guardian™
- Ikiwa utatumia msumari, iweke kwa njia ambayo inahakikisha bidhaa haitoki kwenye msumari


## Maswali ya kuuliza

- Ni vitu gani kwa nyumba unaweza tumia kutundika bidhaa hii?

# Kutupa Guardian™ kwa usalama

## Usiisongeze kwa mwaka mmoja

**1 mwaka**






**Uliza mtaalamu na ufuate maagizo yao**



Usiache kwenye ardhi au barabarani



Usiache kwenye mto, ziwa, au kisima



Usichome

# Kutupa Guardian™ kwa usalama



Karatasi ya kuonyesha mteja





Zingatia

*Shauri mshiriki kuhusu maelekezo ya eneo lenu kuhusu utupaji. Msimamizi wa mradi wako anafaa kukupatia habari hii kabala ya mikutano za kupeana*

## Maneno ya maana ya kuzungumzia

- Tupa bidhaa yako ya Guardian™ baada ya 1 mwaka ya matumizi.
- Kabla ya kuitupa, uliza mtaalamu na ufuate maagizo yao.
- Usiache bidhaa kwenye ardhi au barabarani.
- Usiache bidhaa ndani ya mto, ziwa au kisiwa. Kutupa ndani ya maeneo yenye maji inaweza dhuru wanyama wanaoishi majini.
- Usichome bidhaa.


# Kile unaweza fanya



# Kile unaweza fanya



Karatasi ya kuonyesha mteja




Maneno muhimu ya kuzungumzia

- Unahitaji maelezo yoyote ya ziada?
- Unaweza niuliza maswali wakati wowote.
- Jiskie huru kuja kwangu na maswali yoyote kwa wakati unaokufaa.